# Kiswahili na Usalama wa Chakula: Vikwazo vya Lugha

*Nancy Jumwa Ngowa na Sheila Ryanga*

*Iksiri*

Kufanikisha usalama wa chakula kunategemea ufahamu wa wakulima na jamii ya mashambani[1] kuhusu dhana ya usalama wa chakula, na jinsi inavyojikita katika maeneo yao kimazingira, kimila na kiutamaduni. Uelewa wa wakulima si wa kiutaaluma tu bali pia lugha inayotumika kama inatosheleza mahitaji yao ya ufahamu wa dhana zinazotumiwa, jinsi zinavyofunzwa na kuhusishwa na utamaduni wa jamii zinazohusika. Lugha ina nafasi kubwa katika uhamasishaji na usambazaji wa habari, ujuzi na teknolojia kwa jamii. Lakini lugha haitendi kazi katika ombwe. Lugha hujikita katika utamaduni, mila na uzoefu wa jamii. Hivyo lugha huongoza falsafa, ufahamu na jinsi watu wanavyofasiri ulimwengu wao kijamii, kiuchumi, hata kisiasa. Lugha inayotumika kuhamasisha wakulima, ugumu wa istilahi na dhana ngeni katika harakati za kupata usalama wa chakula na kuondoa umaskini huzua mielekeo na misisimko tofauti kuhusu upokezi ama upuuzaji wa ujuzi na teknolojia mpya. Hii ni kwa sababu ujuzi mpya na dhana ngeni lazima zieleweke kwa wapokezi na zirejelee na kuwiana na falsafa na mila za wanaofunzwa ujuzi na teknolojia hiyo. Huwezi kulazimisha matumizi ya ujuzi na dhana mpya kwa jamii isiyofahamu maana na umuhimu wake.

## 1.0 Utangulizi

Suala la usalama wa chakula linazungumziwa ulimwenguni kote. Hii inatokana na mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yanayotokea duniani. Uongezekaji wa idadi ya watu huongeza mahitaji ya chakula katika nchi zinazoendelea. Kwa nchi zinazoendelea, mahitaji ya kupata lishe bora zaidi na vyakula vya kutosha ni mahitaji ya msingi. Katika nchi hizo, uzalishaji wa chakula na mahitaji haviwiani (Bach, 1978). Kuna mabadiliko katika mifumo ya kilimo na yote haya yanachangia kuifanya mifumo ya kulima ya kijadi kupitwa na wakati. Katika harakati hizi, yule mkulima wa kawaida mashambani nchini Kenya hana nafasi ya kufanikiwa kwa sababu aghalabu ujuzi unatolewa kwa Kiingereza. Mipango ya kufunza na kuhamasisha watu juu ya usalama wa chakula hupangwa kwa minajili ya kuwasaidia raia wengi nchini kuhusu mbinu zinazoweza kuwatoa katika janga la njaa, linalokumba watu wengi nchini Kenya. Lengo kuu ni kujaribu kupunguza matatizo yanayochangia umaskini, upungufu wa chakula kwa familia nyingi, na mbinu za kujiinua kiuchumi. Hili ni jambo linalofahamika kwa Wizara ya Kilimo na Uvuvi katika juhudi zake za kufunza raia juu ya usalama au ustawi wa chakula. Je, katika kushikilia kilimo kama uti wake, ni jambo gani ambalo halijatendeka nchini Kenya katika sekta

[1] Dhana ya mashambani inatumika zaidi Kenya ikiwa na maana ya vijijini kwa Tanzania.

hii ya kilimo ili kufidia utovu uliopo na hali ya kutojitosheleza kwa wakulima wengi mashambani?

Zipo sababu nyingi zinazoweza kutolewa katika kujibu swali hili, zile za kisiasa – kupuuzwa kwa baadhi ya maeneo, kutokuwa na watu wengi waliosoma miongoni mwa wanaoishi mashinani, wengine wakitaja uvivu pia kama sababu, tabia ardhi pia huchangia kwenye sehemu za ukame, na uhaba watalaamu wa kilimo na mabwana shamba na mabibi shamba wanahitajika kutembelea mashamba na kutoa mawaidha kulingana na maeneo tofauti. Baadhi hutoa sababu za kijamii kama kushikilia mila na tamaduni zao dhidi ya nafaka na mimea mingine ambayo pengine hawakuizoea wala kuitumia kama chakula. Miongoni mwa sababu hizi zote, kipengele kinachoshughulikiwa katika makala haya ni lugha. Lugha ina nafasi fulani katika kuzorotesha au kufanikisha juhudi za serikali – Wizara ya Kilimo na mashirika mengine yaliyojitosa kuyainua maisha ya watu kwa kuwafunza mbinu za kiuchumi na chakula. Tungetaka kujua ni lugha gani inayotumiwa na maafisa wa kilimo wanapofunza wakulima mambo haya ya usalama wa chakula katika maeneo mbalimbali ya mashambani. Tungependa kufahamu pia kama kipengele cha mawasiliano na lugha kwa ujumla hufunzwa katika taasisi ya *KIA* na nyinginezo za serikali, yaani ikiwa imeingizwa katika mtaala wao wa mafunzo. Ikiwa haya hayajazingatiwa, basi maafisa hawa hufanyaje kufikisha ujumbe maalumu kwa wateja wao tofauti?

Lugha huandamana na utamaduni, na hali kadhalika mambo ya ukulima. Kila jamii ina vyakula vyake wanavyohusudu tangu enzi za mababu. Kutokana na mabadiliko ya hali ya anga au tabia ardhi, baadhi ya jamii haziwezi kukuza vyakula hivyo tena kwa mbinu wanazofahamu. Hapa ndipo maafisa wa kilimo wanapohitajika kuingilia na kuhamasisha watu kuhusu mabadiliko na mahitaji ya kubadili vyakula na kilimo. Pia, kuelezea watu jinsi ya kujikimu hata wakati usio na mvua ili familia iwe na chakula kila wakati. Hapa ndipo panapoingilia dhana ya usalama wa chakula. Kuna uhitaji wa lugha ya ufunzaji kuwa ile inayofahamika, kama lugha ya taifa – Kiswahili na hivyo kuwa na haja ya kuchambua pia matumizi yake katika mafunzo yanayohusu uhamasisho huu kuhakikisha kila mkulima anafahamu yanayoendelea.

Lugha ina nafasi muhimu katika uhusiano baina ya watu (Gay, 1999). Naye Ferdnand de Saussure (amerejelewa na Gray) anasisitiza umuhimu wa kutambua kwamba lugha ni mojawapo ya asasi za kijamii zisizobadilika haraka. Lugha hutofautiana kwa idadi ya maneno yanayopatikana mawasiliano kuhusu mada fulani mahususi (Gay, 1999). Kulingana na de Sassure, lugha inafinyanga mielekeo, tabia na kuathiri fikra na matendo yetu kwa njia tatu:

1. Maneno katika msamiati (leksikoni) wa lugha hutoleana mipaka. Kila neno linajisimamia na kila neno linabadilika kadri muda unavyopita. Wanaisimu wamedhihirisha kwamba maana ya kila neno miongoni mwa mengine, ni uamilifu miongoni mwao katika vipindi tofauti katika historia ya neno hilo.
2. Kwa sababu msamiati wa lugha huruhusu maana tofauti, hutumika kama njia ya kufasiri ujumbe unaotolewa. Kwa uzoefu wa mwanadamu katika mazingira yake, msamiati wake huegemea tajiriba na maadili yanayopatikana katika jamii yake. Mtu huufikiria ulimwengu wake kulingana na maneno yanayopatikana katika lugha yake. Hili linaenda sambamba na mkulima, lugha na mazingara yake katika ulimwengu wa kilimo.
3. Kwamba tabia inaelekezwa na mwelekeo wa kilugha wa fikra za mtu. Mwanasosholojia Mfaransa, Pierre Bourdieu, ameelezea kinadharia na kihalisi nguvu/uwezo unaopatikana katika lugha (katika Gay, 1999: 304). Uwezo huo husaidia ama kutinga ufasiri wa ujumbe unaowasilishwa kwa yule mpokezi.

Kutokana na hoja hizi za de Sausseur, inawezekana kuwa wakulima tangu uhamasishaji unapofanyika hawajaweza kugeuza tabia ya ukulima na pengine kufikiria ukulima kama biashara kwa sababu ya vikwazo vya lugha? Mazungumzo rasmi juu ya kilimo na masuala ya usalama wa chakula yanafaa kuwa wazi. Lugha yenye utata wa kisarufi, msamiati mgumu, na utohozi wa moja kwa moja wa dhana ngeni na za sayansi na kiteknolojia huweza kughafilisha maana inayowasilishwa kwa wateja na maafisa wataalamu hasa wanapozungumza na wanavijijini wasiobahatika na masomo mengi. Iwe tunajua lugha rasmi ya nchi ama lugha isiyo na hadhi, ikiwa tunajua lugha moja pekee ama nyingi, kwa lugha yoyote tunayoongea na kuandika, tunakabiliwa na leksikografia yake na mfumo wa sarufi uliojumuisha msamiati unaoeleza tu dhana katika tajiriba na utamaduni wa wazungumzaji.

## 2.0 Maelezo ya Dhana ya Usalama wa Chakula

Dhana yenyewe ya usalama wa chakula ni ngumu kufahamika kwa raia wa kawaida, kwani ni changamano. Mara nyingi huambatanishwa na ukulima na utoshelevu wa mavuno na vyakula. Afisa mmoja wa kilimo katika Shirika la *Coast Development Authority* (mahojiano, 8/8/2012), alisema kwamba usalama wa chakula unahusu ujitegemeaji kiuchumi, kiasi cha kuipatia familia chakula mezani kila wakati. Anasisitiza kuwa usalama wa chakula hautegemei sana ukulima bali kuhakikisha kwamba familia haikosi chakula. Unaweza kufikia hili kwa kupata mazao mengi ya kufanya chakula ama, ukauza mazao hayo na

kupata pesa za matumizi, ama kuhakikisha kuwa una biashara ama kazi inayokuwezesha kuepuka njaa na kuwa na chakula kila wakati (CDA, Mombasa - Agosti,2012), na kula chakula chochote mtu atakacho. Anaendelea kusema, kama wakulima wangehamasishwa vyema, wangefahamu kuwa ekari moja inaposhughulikiwa vyema, ingempatia mkulima magunia 13 hadi 18 ya mahindi. Lakini wakulima wengi hulima sehemu kubwa na kuvuna kwa uchache. Dkt. Mwafaida ambaye pia ni afisa wa kilimo na mkuu wa Idara ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Pwani anaelezea usalama wa chakula kuwa ni uzalishaji bora wa chakula. Anasisitiza kuwa ni zile mbinu bora za uzalishaji wa chakula na kilimo kwa ujumla.

Anatilia mkazo kwa kusema kuwa usalama wa chakula ni kuwa na utaratibu maalumu katika kilimo ambao sharti ufuatwe ili kilimo kifanikiwe; ni kuwa na usahihi katika kilimo. Utaratibu huu ni ule wa kuhakikisha kwamba upandaji unafanyika kwa wakati unaofaa, matumizi ya teknolojia iliyoendelea ya kutumia vifaa vya kupiga picha shambani ili kuona ni sehemu gani ya shamba ambayo inahitaji maji au mbolea na ya kiasi gani na kadhalika. Kilimo cha utaratibu maalumu huhakikisha kwamba kila kitu pale shambani, iwe ni kwa mimea au kwa mifugo kinafanyika kitaalamu na kwa uhakika. Kwa mfano, kila dawa ya mimea au mifugo inatolewa kwa kiasi maalumu na kwa wakati unaofaa. Kila kitu kinafanywa kwa kipimo chake cha uhakika. Njia hii ya kilimo inaweza kufanywa na vifaa vya kiteknolojia na mtu ambaye si lazima aende shambani. Yote yanaweza kuendeshwa wakati mkulima yuko ofisini. Kulingana na mtaalamu huyu, njia hii ya kilimo inagharimu wakati wa kuanza lakini huwa ina manufaa makubwa baadaye na ndio njia bora katika kuhakikisha kuna usalama wa chakula. Anasisitiza kwamba lugha inayotumiwa kwa wakulima ni muhimu sana kwani ndiyo huwawezesha kuelewa au kutoelewa njia hizi za ukulima. Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba ili kuwa na usalama wa chakula sharti wakulima wapate mafunzo faafu na matumizi bora ya lugha inayoeleweka kwa wote ili waweze kutekeleza jukumu hili.

Dhana ya Usalama endelevu wa chakula inamaanisha utoshelevu wa chakula kwa kuzingatia uendelezaji wa kilimo, uhifadhi wa mauzo na uzalishaji endelevu kwa mpango. Ni kule kujua misimu na mbegu faafu kwa kila eneo na msimu. Usalama wa chakula pia huashiria ukulima kwa fikra za biashara (Kipindi cha KBC cha `Sikio la Mkulima') dhidi ya kujipatia chakula pekee kama ilivyo wakulima wengi wa aneo la Pwani ya Kenya. Lakini hata kuwa na fikra hizi huhitaji uhamasishaji kwa lugha inayofahamika.

Ni dhihiri kwamba dhana ya usalama wa chakula inakanganya na uelewa wakc unahitaji ufasiri wa hali ya juu. Dhana hii inapaswa ieleweke katika lugha ya Kiingereza kisha iweze kutafasiriwa katika lugha ya Kiswahili. Ni jukumu la anayefasiri dhana hii kuielewa katika lugha ya Kiingereza kisha aweze kuifasiri katika lugha ya Kiswahili. Iwapo anayefasiri dhana hii hajaielewa vyema katika lugha ya Kiingereza basi hatafaulu katika kuitolea maelezo yake katika lugha ya Kiswahili. Dhana hii inavyotafsiriwa kama Usalama wa chakula pia haitoi maana ya moja kwa moja. Kwa hivyo dhana hii inahitaji kutafsiriwa na kufasiriwa, zoezi linalohitaji ufahamu wa lugha si ya Kiingereza tu bali pia Kiswahili kama lugha pokezi ya wateja. Usalama wa chakula unahusu kuwasilisha masuala ya kilimo kwa njia inayovutia. Hili hufanyika kwa matumizi ya lugha inayovutia,

**3.0 Mafunzo kwa Wakulima**: "*Elimu haina mwisho*"

Shule za wakulima ni maarufu ulimwengu mzima (IFPRI, 2010). Katika mafunzo ya kilimo nchini Kenya, lugha zilizopendekezwa na wizara ya kilimo ni Kiingereza na Kiswahili. Walimu wa kilimo wanatakiwa kuwa na ufahamu wa Kiingereza na Kiswahili na uwezo wa kubadili msimbo wakati wowote ule inapobidi. Changamoto ni kwamba, istilahi nyingi za Kiingereza hazina visawe vyake katika lugha ya Kiswahili kwa hivyo inabidi zitoholewe. Istilahi za kutoholewa huwa hazina maana yoyote kwa lugha ya Kiswahili na hupotosha.

Walimu wanapoenda kuwafundisha wakulima wanakiri kwamba changamoto kuu huwa ni mawasiliano baina yao na wakulima. Kwa wale wenyeji wa eneo mahususi, wanalazimika kutumia lugha ya mama katika maelezo wanayoyatoa kwa wakulima. Lakini kwa wale ambao hawatoki eneo hilo, inawabidi watumie Kiingereza ili kuwasiliana kwani Kiswahili huwa ni kigumu kwao na hawaeleweki kwani istilahi zinazotumika huwa zinapotosha.

Inabidi walimu wasome na kuelewa vizuri kile wanachotaka kufundisha kisha wakieleze kwa lugha rahisi iwezekanavyo ili waweze kueleweka. Walimu wanaoendesha mafunzo ya kilimo huwa wanafundishwa kwa lugha ya Kiingereza katika masomo yao kwa hivyo mfumo wa elimu unaosisitiza lugha ya Kiingereza hutoa hali ngumu kwa walimu hawa wanapokuwa nyanjani wanapotakiwa kufundisha katika Kiswahili ambacho hawajakipitia kiakademia.

Ili kueleweka vilivyo walimu hawa hutumia mbinu za uoni na majaribio. Kila kazi ya shambani inayofanywa lazima ifanyiwe majaribio ili iweze kuonekana waziwazi. Wakulima huwa wanaelewa kwa kiasi fulani kwa kuona kinachofanyika hata kama lugha hawaipati vizuri.

Wakulima lazima waone mbolea hizo hata kama hawazijui majina yao ya kisayansi. Huwa wanaangalia rangi ya mbolea fulani na kujua rangi fulani ni ya kutumiwa wakati wa kupanda, rangi fulani wakati wa kupalilia, na kadhalika bila kujua majina yao hasa. Changamoto hapa ni kama mbolea zina rangi za kufanana.

Maafisa wa kilimo wana jukumu zito na lenye changamoto kubwa. Maafisa hawa hufunzwa masomo haya ya kisayansi kwa Kiingereza na wengi wao hawajajua Kiswahili wala kueleza katika mafunzo hayo. Mafunzo haya huwa yamesheheni istilahi za kisayansi ambazo ziko katika Kiingereza. Maafisa na walimu wa kilimo huwa na jukumu la kutafsiri istilahi hizi katika lugha ya Kiswahili ili zieleweke kwa wakulima. Kwa mfano, dhana ya usalama wa chakula yenyewe ni kizungumkuti kwa wakulima, na wananchi kwa ujumla.

Maafisa wa kilimo wanakubaliana kwamba wakulima wengi hawajasoma. Kulingana na Dkt. Mwafaida wa Chuo Kikuu cha Pwani, karibu asilimia 80 ya wakulima hawana elimu ya msingi ya kusoma na kuandika. Anaongeza kwamba asilimia 60 ya idadi ya watu nchini Kenya hutegemea kilimo ili kukidhi mahitaji yao ya chakula. Hivi ni kusema kwamba, watu wengi nchini wanategemea wakulima kuwalisha na wakulima hawa hawana elimu ya kukuza mimea.

Ukosefu huu wa elimu una madhara mengi kwani huathiri mawasiliano kwa kiasi kikubwa. Kulingana na maafisa wa kilimo Chuo Kikuu cha Pwani, ukosefu wa elimu na matumizi ya lugha faafu hufanya wakulima watumie dawa kidogo au kupita kiasi kwa sababu ya kutoelewa maelezo na umuhimu wa vipimo sahihi vya dawa. Kuzidisha dawa katika mimea au mifugo hudhuru vibaya na hali hii inaweza kuua mimea au mifugo. Kwa upande mwingine, kipimo kidogo cha dawa husababisha ugonjwa kuwa sugu na kutosikia dawa tena katika mimea au mfugo mahususi. Hivyo basi sharti maelezo haya ya dawa yatolewe kwa lugha itakayoeleweka kwa wakulima hawa.

Shule za nyanjani za wakulima ni njia mojawapo muhimu sana ya kupambana na umaskini na kuhakikisha kwamba kilimo kinaboreshwa. Wakulima wanapata ujuzi ambao unawasaidia katika ukulima (Christoplos na Kidd, 2000). Shule hizi ziko kote ulimwenguni na zimekuwa mashuhuri sana kwa sababu ya ile haja ya mataifa kutaka kuondoa utegemezi wa chakula na umaskini. Kulingana na Braun na wenzie (2006) shule hizi zinapatikana katika zaidi ya nchi 78 za ulimwenguni na zinaendelea kupanuka. Kulingana na ripoti ya FAO/KARI/ILRI (2003), nchi ya Kenya ina zaidi ya shule za wakulima elfu

moja (1000) na zaidi ya wakulima elfu 30 ambao wamefuzu katika shule hizi. Shule hizi ni muhimu sana. Hata hivyo, shule hizi zinakumbwa na changamoto ya mawasiliano baina ya walimu na wakulima hasa kwa upande wa lugha.

Mara nyingi maafisa wa kilimo huendesha mafunzo katika shule hizi kwa lugha ya Kiswahili ambayo hawana umahiri nayo na baadhi hutumia lugha ya Kiingereza. Wanaotumia lugha ya Kiswahili huwa wanasoma maelezo yao kwa lugha ya Kiingereza kisha wakafasiri katika lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo, hawaandiki maelezo yoyote baada ya kutafsiri bali huweka kumbukumbu hizi kichwani. Tafsiri hizi huwa na upungufu. Wakati mwingine wakulima hawaelewi wanachoambiwa na aghalabu wanazidisha kipimo cha dawa fulani wakidhani kwamba waliyoambiwa ni kidogo sana. Wakati mwingine kama hawajaelewa wanakadiria kwa mfano wakiona ng'ombe ni mkubwa wanampa dawa nyinyi.

Hali hii mara nyingi hutokea kwa sababu wakulima hawaelewi au hawajui kusoma vifaa vya kitaalamu vya kupimia dawa kwa hivyo inabidi maafisa watumie vifaa vingine vinavyofanana na hivyo kama mikebe na kujaribu kukadiria kiasi cha dawa inayohitajika. Haya yote yanaletwa na kutofahamu maelezo wanayopewa ambayo yamejaa istilahi za kutoholewa.

Ni muhimu kutambua kwamba ijapokuwa wengi wa wakulima hawa hawana elimu ya msingi, wanaelewa vyema Kiswahili. Kikwazo zaidi hapa ni maafisa wa kilimo kushindwa kutafsiri yale masuala ya kilimo kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Kama ilivyotangulizwa hapo awali, maafisa hawa hupata masomo haya katika lugha ya Kiingereza na ni vigumu kuweza kuyatafsiri katika Kiswahili.

### 4.0 Vikwazo vya Lugha

Gray (1999) anaendeleza fikra kuwa uhuru wa kiisimu na ubunifu wa kiisimu huweza kujenga vikwazo miongoni mwa makundi ya jamii, na kukanganya ufahamu wao, hali ambayo uhuru huo huweza kuwapa uwezo jamii nyingine na kuwapanua uelewa wao. Uteuzi wa lugha na maneno fulani katika lugha huongozwa na uzoefu wa matumizi katika jamii, hivyo hatuwezi kuwalaumu maafisa wa kilimo wanaotumia Kiingereza kufunza wateja wao kwa sababu walijifunza elimu hiyo kwa Kiingereza. Lawama pengine ni kwa Wizara kutozingatia kufunza Kiswahili kama somo katika taasisi ya kilimo, ambapo lugha hii imekuwa ya taifa na kutumika kwa mapana kwa miaka mingi. Hili ni mbali na kutambua kuwa maafisa hawa watapelekwa kufanya kazi kokote nchini, miongoni mwa hata wale ambao hawakijui wala hawawezi kuongea

Kiswahili. Hii huwa changamoto kubwa katika kutekeleza wajibu wao. Si ajabu basi kwamba, wakati mwingine inawabidi kuchanganya ndimi katika juhudi za kutumia Kiswahili na kupatikana kwa sarufi potofu kwa kutojua Kiswahili na mnyambuliko wala mfumo wake.

Matumizi ya lugha potofu kwa kawaida si ya kimakusudi; ni kukosa ujuzi wa lugha, jambo ambalo halikubaliki siku hizi ambapo mtu anaweza kujifunza mbinu za kazi yake, hata lugha kupitia teknolojia mpya. Itakuwaje serikali na Wizara ya Kilimo kubaki nyuma ya Katiba, kuhusu Kiswahili? Lugha inayotumika kuhamasisha kuhusu usalama wa chakula mradi iwe chombo cha kuleta mabadiliko katika kilimo, mbinu na mielekeo na hatimaye kuchangia uboreshaji wa uchumi, hivyo kuondoa umaskini. Yafaa kuwahamasisha wakulima wafikirie ukulima kama biashara ya kujipatia pesa, wala si kwa chakula cha familia tu ghalani, kama alivyosema afisa wa Kilimo wa CDA na yule wa Idara ya Sayansi Chuo Kikuu cha Pwani waliorejelewa hapo awali. Lugha inayotumiwa iafiki fikra zao na kuwatoa katika wa kilimo chao cha kitamaduni hadi mifumo mipya itakayokuwa na tija.

## 4.1 Lugha ya Mbolea

Katika kilimo hasa cha mimea, kila mmea unahitaji mbolea ya aina fulani ili kufanikisha ukuaji na mavuno bora kwa mmea huo (van Slyke, 2010). Mbolea maarufu zaidi ni za Kemikali zenye majina ya kisayansi. Wakulima wengi hawana ufahamu wa majina haya na matumizi ya mbolea kwa jumla. Wanapopewa mafunzo ya jinsi ya kukuza mimea/mazao fulani au hata mifugo, wanalazimika kutoa mafunzo hayo kwa kufasiri mbolea hizo, kwa mfano: protini ya ng'ombe, (kipindi cha radio). Hata kama istilahi hizi zinakubalika katika lugha ya Kiswahili ni vigumu kwa mtu wa kawaida kufahamu zina maana gani. Mbolea zingine zinatamkwa kwa majina ya Kiingereza kwa sababu maafisa wa kilimo wanashindwa kupata visawe vyake katika lugha ya Kiswahili. Angalia mifano ifuatayo:

(a) Mbolea ya *potassium*
(b) Mbolea ya *nitrogen*
(c) Mbolea ya *phosphorus*
(d) Mbolea ya *calcium compounds*.

Majina kama hayo huzidi kuwapotosha watu wa kawaida ambao hawajui lugha ya Kiingereza. Hiki ni kikwazo katika ukulima. Iwapo watu hawaelewi maelezo hayo kwa sababu ni ya kisayansi mno na istilahi zinazotumika hazieleweki, basi ni vigumu sana kuweza kutimiza malengo ya utoshelevu wa chakula kwa sababu maagizo hayatafuatwa vizuri. Ni muhimu kwa wanalugha kuibua istilahi

za asili za lugha ya Kiswahili ili kufanikisha uelewa na ufanisi wa kilimo na usalama wa chakula.

### 4.2 Suala la Visawe

Uwazi wa maafisa kutumia Kiingereza, inapobidi Kiswahili na zaidi ikilazimu lugha ya Kienyeji ikiwa afisa yuko katika eneo la wakulima amapojua lugha yao. Tatizo katika lugha nyingine isipokuwa Kiingereza ni kupata visawe toshelevu vya dhana zile za kiteknolojia na kisayansi. Vipindi vya televisheni vya kuomba msaada na mafunzo ya ukulima, huwapita watu wengi ambao hawana televisheni, hasa katika maeneo ya shambani, ambako hakuna maendeleo mengi wala ufahamu au upatikanaji wa televisheni.

Mafunzo ya redio, (Kipindi cha wakulima cha 'Sikio la Mkulima') ambayo yatarajiwa kusikilizwa katika taifa lote, bado matatizo ya matumizi ya lugha ya Kiswahili hayajafanya Wizara ya kilimo kufunza Kiswahili kwa maafisa wao wanaokutana na wakulima nyanjani. Ni wazi lugha inayotumiwa redioni kwa vipindi vya wakulima si tofauti na ile inayotumiwa mashambani na maafisa wanozuru wakulima huko. Maafisa ni wale wale.

### 4.3 Kuchanganya Msimbo

Kama ilivyotaja hapo awali walimu wa mafunzo ya nyanjani ya wakulima hawafahamu Kiswahili vyema na baadhi hutumia Kiingereza. Kwa hali hii, kuchanganya msimbo ndilo kimbilio lao ili kuwasilisha dhana wanazowafunza wakulima. Katika kueleza magonjwa ya mimea na mifugo, tunapata:

(a) Magonjwa ya *fungal*
(b) Magonjwa ya *bacteria*
(c) Magonjwa ya *Viral.*

Walimu wa kilimo wanakiri kwamba ni vigumu kueleza magonjwa haya mpaka yaeleweke. Ili kujaribu kueleweka, inabidi walimu hawa wawapeleke mashambani wakulima ili wawaoneshe mimea au mifugo yenye magonjwa haya. FAO (2001) inapendekeza kwamba wakulima wafundishwe masomo ya ukulima na teknolojia yake kwa njia ya uhusishi. Hivi ni kusema kwamba wakulima hawa wanapaswa wajihusishe kikamilifu mashambani katika mambo mbalimbali, kwa kuyaona na kuyashughulikia. Kwa mfano, kuna ugonjwa wa bakteria unaoitwa '*water rot*' ambao unashika mimea na unaposhika mifugo ugonjwa huo unaitwa '*hoof rot*' au '*foot rot.*' Walimu wa kilimo wanasema kwamba inabidi watumie mbinu zao wenyewe ili kuhakikisha kuwa wakulima wameelewa. Kwa sababu wakulima ni watu wazima, inabidi zile mbinu za

kufundishiwa kilimo zilenge watu wazima. Davis na Place (2003) wanasema kwamba wakulima wafundishwe masomo ya kilimo kwa mbinu za watu wazima (ngumbaro) na wanasema mbinu hizi zihusishe kufanya majaribio pale shamhani. Kwa mfano, wanapotajiwa majina haya ya Kiingereza wanawapeleka wakulima kule shambani wakaone magonjwa yenyewe ndio wajue jinsi ya kuyanyunyizia dawa kwa matendo. Kwa kweli, wakulima hawa hawaelewi lugha ya Kiingereza inayotumiwa kwa magonjwa haya. Pia hawawezi kukumbuka majina haya baadaye wanapotakiwa kuyaeleza kwa wengine. Hii ni kwa sababu majina haya ni mageni kwao na si rahisi kujinasibisha nayo. Walimu wa wakulima hawa wanakiri kwamba lugha ni kikwazo kikubwa sana katika mawasiliano yao na wakulima. Walimu hawa wanasema kwamba sharti kuwe na lugha mwafaka itakayotumiwa katika kufundisha wakulima ili kufanikisha kilimo.

Majina ya dawa za mifugo na mbolea huwa yameandikwa kwa Kiingereza na inawabidi walimu wayatamke kwa lugha hiyo ya Kiingereza. Ikumbukwe kwamba wakulima hawa ni wale ambao wengi wao hawana elimu na hawajui kusoma na kuandika. Majina haya yanapotamkwa kwa Kiingereza huwa ni kizungumkuti kwao. Hawaelewi yanamaanisha nini na wayahusishe na kitu gani. Baadhi ya majina haya ya dawa yaliyotolewa nyanjani ni:

(a) *Antricol* ambayo ni dawa ya mimea ya *fungal*
(b) Nizam ni dawa ya minyoo ya mifugo
(c) *Ridomil* ni dawa ya *fungal*
(d) Karate ni dawa ya mimea ya wadudu
(e) *Politrin* ambayo ni dawa ya wadudu
(f) *Biosol* ambayo ni dawa ya kutibu macho ya kuku.

Kulingana na walimu wa wakulima dawa hizi zinatamkwa kwa lugha ya Kiingereza halafu walimu hawa wanawaonesha dawa hizi ili kufanikisha kuelewa. Bila shaka wakulima hawa huwa hawaelewi ile lugha ya dawa hizi ndio maana inabidi waonyeshwe dawa zenyewe au mikebe ya dawa hizi ili watazame na kuweka mikebe hiyo akilini mwao. Wakati mwingine wanapotaka dawa hiyo wataitambua kwa mkebe wala sio jina lake kwa sababu jina hilo hawawezi kulihusisha na kitu chochote wanachokijua katika mazingira yao. Changamoto ni kwamba kampuni ya dawa hiyo inapoamua kubadilisha muundo au rangi ya mkebe wakulima hawa hawataweza kuutambua tena mpaka waelezewe kuhusu mkebe huo mpya. Ni bayana kwamba lugha mahususi ambayo mkulima anaweza kujinasibisha nayo itumike ili wakulima waelewe vyema. Lugha ambayo ni ya taifa ni Kiswahili. Wakenya wengi hata wale

ambao hawana elimu wanaweza kuongea Kiswahili na ni lugha ambayo wanaweza kujitambulisha nayo.

### 4.4 Mifano mingine ya Kuchanganya Misimbo

(i) "*Tissue culture* ni *simple process* ya kuchukua mbegu na kuzizalisha ndani ya chupa."

(ii) Katika kueleza jinsi ya kupanda migomba afisa anasema, "unachimba shimo hii na kumwaga *saka* ya kawaida hii ni *conventional saka.*"

(iii) Afisa mwingine katika kipindi cha Sikio la mkulima asema anapozungumzia ukulima wa nyuki, "...kuna aina ya wanyama wengine wanaoitwa *honeyberger...*"

(iv) "Lazima unapotoa asali kwenye mzinga uwe na *protective clothes*".

(v) "..*Tissue culture* ni *lower level technology* ikifananishwa na *GMO* inayochukua muda mrefu"

(vi) Kuna maneno ya Kiingereza yaliyo magumu hata kwa afisa kuyaeleza kwa Kiswahili

*(vii) "Acid soils which contains free alumminum which inhibits the growth...'*

*(viii) (Kipindi cha sikio la mkulima).*

### 4.5 Utohozi wa moja kwa moja

Hufanyika hasa wakati wa kufundisha kuhusu aina na majina ya mbolea katika mafunzo kwa wakulima kwa mfano, kuna Kuna mimea mingine ambayo hutumia majina ya kisayansi yaliyotoholewa ambayo huwa hayaeleweki kwa wakulima na hupotosha maana. Ripoti ya KEFRI ya Ustawishaji na Usimamizi wa Miti yenye Thamani Mashambani (2004) inatoa orodha ya mimea yenye majina ya kisayansi yaliyotoholewa kama ifuatavyo:

| **Jina la mmea lililotoholea** | **Jina la mmea la kisayansi** |
|---|---|
| Moringa | *Moringa oleifera* |
| Lukina | *Leucaena Leucocephalla* |
| Kaliandra | *calliandra calothyrsus* |
| Glirisidia | *Gliricidia sepium* |

Ni dhahiri kwamba majina ya mimea hii yaliyotoholewa kutokana na majina yake ya kisayansi ya asili na kupelekwa katika lugha ya Kiswahili, hayatoi maana yoyote katika lugha ya Kiswahili. Mara nyingi wakulima hawawezi kuhusisha mmea na jina lile walilopewa. Kwa mfano, mmea wa moringa ni mti ambao unamea kwa wingi sana katika maeneo ya Pwani ya Kenya (Shackleton

na wenzie, 2009) na huwa unatumika sana na Wamijikenda kama mboga inayopikwa pamoja na mchunga. Mmea wa moringa pia unajulikana sana kwa kutibu na kuzuia magonjwa. Kwa wenyeji wa Pwani hasa Wamijikenda, ukiwatajia jina la moringa hawatajua unazungumzia mmea gani hata kama ni ule uliopo hapo bomani kwao kwa sababu jina hilo ni geni kwao. Mti huu wanaujua kwa lugha yao ya mama kama 'mzungwi'. Kwa hivyo ukiwatajia 'moringa' watasema hawaujui lakini ukiwatajia 'mzungwi' watakuonesha mara moja.

Majina haya ya kisayansi yanawakanganya. Mimea ambayo wanaijua kwa majina yao ya lugha ya mama hawaijui wanapotajiwa katika lugha ya sayansi. Ni vigumu kuweza kuwasiliana katika hali hii. Katika kipindi cha runinga mwasilishaji mmoja alisikika akisema yafuatayo: "ng'ombe wanahitaji *protini* nyingi ili wajenge mifupa" (TV – citizen -3/6/2012). 'Proteni' ni dhana ambayo haieleweki kwa mtu wa kawaida hasa mazingira ya uswahilini kwa sababu hawezi kuinasibisha na kitu chochote katika mazingira yake.

### 4.6 Masuala ya Sarufi

#### 4.6.1 Utata wa maana katika mashina ya majina

Kuna mimea mingine ambayo iko katika lugha mama na imetafsiriwa katika Kiswahili ambapo maana inabadilika kabisa. Kwa mfano 'mtsunga' katika lugha ya Kigiryama ni kule kuwa na maumivu 'uchungu' na ikiwa katika lugha ya Kiswahili 'mchunga'ni kule kuangalia kitu fulani mfano mifugo, au wafuasi iwapo ni mchungaji wa kanisa. Maana hizi zinahitiliafiana katika maelezo na wanaoelezwa. Mfano huu uliopatikana nyanjani unadhihirisha kwamba kutafsiri kisisisi kwa majina ya mimea kutoka lugha ya kienyeji hadi lugha ya Kiswahili pia kunatatanisha maana, na istilahi inayoibuliwa haina uhusiano na ile ya awali. Katika lugha yoyote ile usahihi wa sarufi huleta umaarufu katika matumizi ya lugha na kuwasilisha maana bila utata wowote.

#### 4.6.2 Sarufi Potofu

Kwa mfano, katika usemi ufuatao kutoka katika kipindi cha 'sikio la mkulima' '.....kuna sehemu nyingi '*ambaye*' wanapatikana watu wakifuga nyuki' Kirejeshi 'ambaye' hapo juu si sahihi katika muktadha huu.

### 5.0 Mapendekezo

Baada ya maelezo na ufafanuzi huo, makala haya yanapendekeza yafutayo:
Mosi, serikali na Wizara ya kilimo iunde sera ya kujumuisha mafunzo ya somo la Kiswahili katika mitaala yake ya kilimo katika Taasisi ya Serikali ya Kilimo kule Kabete (KIA) ili maafisa wa kilimo waweze kutumia lugha ya Kiswahili wanapofunza wakufunzi wanaokwenda kufunza kwingine.

Pili, kuwe na nafasi ya wakalimani wakati wa mafunzo kwa wakulima mashinani ili maelezo yaweze kufanikiwa. Tatu, ongezeko la wanasayansi wa kilimo na chimbuko la teknolojia vimezua maandishi mengi kwenye majarida na vitabu ambavo yanahitaji kutafsiriwa kwa Kiswahili ambayo ni lugha ya wengi ama lugha za kienyeji nyinginezo ili watu wengi waweze kuyatumia na kuwanufaisha. Kuwe na miradi ya kutafsiri nyaraka mbalimbali za kisayansi na teknolojia zinazofunza usalama wa chakula.

Nne, taasisi za vyuo vikuu zifanye utafiti wa masuala ya kilimo endelevu na kufanya mbinu za uundaji wa istilahi na uandishi wa makamusi ya kilimo na malighafi nyingine ya ujuzi huu kwa Kiswahili. Tano, wakulima wahusishwe katika uundaji wa istilahi katika mbinu za mawasiliano na matayarisho ya vitabu vinavyotumika kwa wakulima nyanjani katika Kiswahili. Sita, matayarisho ya vitabu vinavyotumika kwa mafunzo ya wakulima nyanjani yawe kwa Kiswahili ili iwe rahisi kueleweka kwa watu wa kawaida.

## 7.0 Hitimisho

Makala haya yameeleza jinsi vikwazo vya lugha vinavyoweza kuzuia na kuzorotesha uelewa wa mafunzo kwa wakulima. Maafisa waliohojiwa wanadhihirisha kuwa, ukiukaji wa sarufi sahihi, utohozi wa moja kwa moja wa maneno ya Kisayansi na kuchanganya misimbo kwa watu wasio na kisomo huondoa ari na kuathiri juhudi za ukulima na hasa usalama wa chakula.

**Marejeo**

Bach, R. (1978). "Developments in Potassium Research." Potassium Research-Review and Trends. Congress on the Occasion of the 25th. Anniversary of the Scientific Board of the International Potash Institute. International potash Institute, Bern/Switzerland: CH-3048 Worblaufen.

Bourdieu, P. (1991). Language and Symbolic Power. Ed. John B. Thomson, trans. Gino Raymond and Matthew Adamson. University Press, Cambridge: Harvard

Braun, A. J. Jiggins, N. Roling, Van Den H. Berg, na P. Snijders (2006). *A Global Survey and Review of Farmer Field School experiences.* Nairobi: International Livestock Research Institute.

Christoplos na Kidd. (2000). A *guide for Monitoring, Evaluation and Joint Analyses of Pluralistic Extension Support.* Lindau: Neuchantel Group.

Davis, K na N. Place. (2003). Non-Governmental Organization as an Important Actor in Agricultural Extension in Semi-Arid East Africa. *Journal For International Agriculture and Extension Education* 10 (1): 31-36.

Davis, K., E. Nkonya, E. Kato, D. Mekonnen, M. Odendo, R. Miiro na J. Nkuba. (2010). *Impact of Farmer Field Schools on Agricultural Productivity and Poverty in East Africa.* A Discussion Paper of IFPRI (International Food Policy Research Institute) .

FAO (2000). Progress report – 2001. *Farmer Innovations and New Technology options for Food Production, Income generation, and Combating Desertification.* KEN/99/200. Nairobi: FAO.

FAO/KARI/ILRI(FAO/Kenya Agricultural Research Institute/International Livestock research Institute). (2003) *Farmer Field Schools: The Kenyan Experience.* Report of the Farmer Field School Stakeholders' Forum, March 27, Nairobi: ILRI

Gay, C. W. (1999). "The Language of War and Peace," Encyclopedia of Violence, Peace, and Conflict.ed. Lester Kurtz (San Diego; Academic Press) Volume 2, 303-312.

KEFRI. (2004). Ustawishaji na Usimamizi wa Miti yenye Thamani Mashambani. Alisei Italy, EAWS, KEFRI: Nairobi

Shackleton, C. M. Pasquini, na A. Drescher. (2009). *African Indigenous Vegetables in Urban Agriculture.* Earthscan Duncan House. London.

Tisdale, S. na W. Nelson. (1975). *Soil Fertility and Fertilizers.* New York: Macmillan Publishing House.

Van Slyke, L. (2010). *Fertilizers and Crop Production.* Agrobios India. Jodhpur.